



# *Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo*

## **1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01- 10 MEI, 2024 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 11- 20 MEI, 2024**

### **1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01- 10 MEI, 2024**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika kidogo wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilidhohofika. Hali hii ilisababisha ukanda mvua (ITCZ) kusogea kaskazini na kuwepo katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria. Joto la bahari katika eneo la Kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi lilikuwa la juu ya wastani. Hali hii ilisababisha kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa kwenye eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi ambayo iliimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani. Kimbunga "HIDAYA" ni miongoni mwa migandamizo midogo ya hewa iliyosababisha mvua kubwa na vipindi vya upepo mkali katika maeneo ya ukanda wa pwani.

### **1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01- 10 MEI, 2024**

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria, magharibi, nyanda za juu kusini-magharibi, maeneo ya nyanda za juu kaskazini-mashariki na katika maeneo ya ukanda wa Pwani. Maeneo ya ukanda wa kati na kusini yalikuwa makavu kwa ujumla.

## **2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11- 20 MEI, 2024**

### **2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 11- 20 MEI, 2024**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kudhohofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kusogea kaskazini na kuwepo katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria na Magharibi mwa Nchi. Joto la bahari katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa chini kidogo ya wastani

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

wakati lile la magharibi mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kusababisha vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani.

## **2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 11- 20 MEI, 2024**

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Vipindi vya ukavu kwa ujumla vinatarajiwa.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Mvua zinatarajiwa katika maeneo machache hasa yale yenye miinuko.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Mvua nyepesi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Vipindi vya ukavu kwa ujumla vinatarajiwa.

Imetolewa na;

## **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)